

Ukweli Hauna Kutu

Pambazuko

Toleo Namba 016

Jumatatu Oktoba 24-30, 2022

Nape, hebu tupumzishe kidogo Uk. 4

**Wachina
waongeza
umasikini
Uk. 5**



Rostam Aziz

Wizi wa kutisha Pride

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Katiba mpya iwezekane sasa

IJUMAA iliyopita - Oktoba 21, Rais Samia Suluhu Hassan, alipokea ripoti ya Kikosi Kazi alichokiunda ili kukusanya maoni na mapendekezo kutoka kwa wananchi kwa lengo kuu moja; kuiweka Tanzania salama na bora zaidi kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kikosi hicho kilichokuwa na wajumbe kutoka kada mbalimbali, kilifongozwa na mwenyekiti wake, Profesa Rwekaza Mukandara, ambaye ni mbobezi katika siasa na demokrasia, kilijumuisha pia wajumbe kutoka maeneo mbalimbali ikiwemo wanasiasa, asasi za kiraia, na makundi mengine, kilizunguka nchi nzima kusikiliza matamano ya Watanzania kuhusu hatma ya nchi yao.

Katika mapendekezo yaliyokusanywa, ripoti imegusia masuala mbalimbali, kuanzia usawa wa jinsia, demokrasia, muundo wa Tanganyika na Zanzibar, suala la katiba mpya na zaidi sana kufunguliwa kwa milango ya fursa kwa Watanzania wengi zaidi.

Ripoti hiyo, kimsingi, imejaa mapendekezo kutoka kwa wananchi waliohojiwa kueleza nchi wanayoitaka.

Hata hivyo, suala la Katiba mpya lilichukua nafasi kubwa, huku wengi waliohojiwa wakitamani kuona kunakuwepo kamati maalum ya kupitia kile kilichokusanywa kutoka kwa wananchi - wakati wa mchakato wa kupata katiba mpya.

Wanapendekeza kwamba Rasimu ya Katiba ya Jaji Warioba na Katiba Inayopendekezwa, vikusanywe na kuchambuliwa upya na wataalamu wa sheria na maeneo mengine wanaoaminika kwa jamii ili watoe majumuisho

yanayobeba mawazo ya wananchi.

Pamoja na kwamba wapo baadhi waliopendekeza kuanza upya kwa mchakato wa kupata katiba mpya, sisi katika Pambazuko tunaona ni vyema na haki kwenda na idadi kubwa ambao wanapendekeza kupitiwa upya yaliyofanywa na Tume ya Jaji Warioba.

Uhakika tulionao ni kwamba kuanza upya kwa mchakato kutaigharimu nchi fedha nyingi mno na pia muda, wakati mapendekezo ya wananchi yapo, hivyo hakuna haja ya kurejea kile kilichofanywa.

Ikiwa hayo yataridhiwa, Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kufanya hivyo, kwani Afrika Kusini mwaka 1992 ilishindwa kupata katiba mpya kutokana na mvutano wa makundi, hasa wanasiasa na ndipo iliamuriwa kuwepo kwa katiba ya mpito, huku kamati maalum ya wataalamu ikiundwa na hatimaye ikaja na katiba inayoelezwa kuwa bora zaidi Afrika.

Mbali na Afrika Kusini, majirani zetu hapo Kenya mwaka 2005, serikali iliyoanzisha kura ya maoni kuhusu namna bora ya kuendesha nchi, ilishindwa kura ya maoni na kuridhia kamati maalum kupitia yale yaliyokusanywa na kupatikana kwa katiba inayotumika sasa, ikiwa imesheheni mazingira ya demokrasia pana, hata kama bado inabeba upungufu ambao unaweza kurekebishika.

Hivyo basi, ni vyema tukaamua kuwa na kamati maalum itakayopitia yaliyokusanywa na kuchakatwa na Tume ya Jaji Warioba ili kuwa na katiba mpya yenye kuondosha chembe za ukakasi katika masuala mbalimbali.



Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Tupinge mfumo wa elimu unaomezsha propaganda.

Tuhoji wimbo tunaousikia kila siku kutoka kwa baadhi ya wanasiasa kwamba elimu ijenge uzalendo. Siyo kazi ya elimu kujenga uzalendo. Kazi ya elimu ni kuzaa vijana wenye kipaji na ustadi wa kudadisi dhana zote pamoja na dhana ya uzalendo na utaiifa. Kazi ya elimu ni kufikirisha, siyo kukumzesha fikra – Prof. Issa Shivji.

Nape, hebu tupumzishe kidogo

Na Dkt. Bullet RUHINDA

NAPE Nnauye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, amenukuliwa na chombo vyombo kadhaa vya habari akidai kwamba anatamani mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa iruhusiwe, maana inakisaidia chama tawala kuliko hali ilivyo sasa ya kuzuiwa.

Ni tamanio jema, ila linashangaza limetoka kwa nini muda huu? Tena limetoka kwa mtu ambaye kwa namna moja au nyingine ni miongoni mwa viongozi walioshiriki kuondoa haki hiyo ya vyama vya siasa ambayo ni ya kikatiba.

Wakati nakiendelea kuitafakari kauli hiyo wa Nape, nikakutana na video fupi ya mahojiano kati ya muasisi wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere na mwandishi mmoja wa Uingereza aliyemuuliza kama Tanganyika ilikuwa tayari kwa uhuru mwaka 1959!

Majibu ya Mwalimu yalikuwa kwamba, “Huwezi kuja nyumbani kwangu ukaniibia koti langu, kisha nikija kukudai koti langu unaniuiza kama koti hilo litanifaa! Koti lilikuwa la kwangu kabla hujaliiba na litaendelea kuwa la kwangu hata kama unalo wewe hivyo, huna haki ya kuniuliza kama linanifaa au la, zaidi tu unirejeshee hali yangu!”

Majibu haya ya Mwalimu Nyerere ni mujarabu kwa tamanio la Nape. Serikali iliondoa haki ya kikatiba na kisheria ya vyama vya siasa kufanya siasa kupitia mikutano ya hadhara. Hakuna kifungu chochote cha sheria au katiba kinachokubaliana na marufuku hiyo.

Ni ajabu sasa muhusika katika marufuku huyo kuja na maelezo juu ya uzuri wa mikutano ya hadhara. Anachotakiwa kufanya ni kurejesha haki hiyo ya kikatiba kwa vyama maana iliyorwa.

Sababu mojawapo anayosema Nape kuhusu kuondolewa wa marufuku hiyo ni kwamba anadhani mikutano itakisaidia chama tawala CCM (Chama



Mhe. Nape Nnauye

Cha Mapinduzi) kuliko ilivyo hivi sasa. Inashangaza kwamba anashauri mikutano irejeshwe siyo kwa sababu ni haki ya kisheria ya wananchi kupitia vyama vyao ikiwemo CCM, bali kwa sababu chama chake kitanufaika! Ajabui.

Wakati marufuku ya kwa mikutano ya hadhara inatangazwa, hakuna wananchi walioulizwa maoni yao. Inashangaza pia kwamba sasa aliyehusika na marufuku hiyo yupo kwenye vyombo vya habari kueleza uzuri wa mikutano hiyo bila kueleza uharamia uliotumika kuipiga marufuku.

Kama wasikilizaji wake tungependa kumuuliza Nape kama hayo ni mawazo yake binafasi na kama hayapingani na msimamo wa chama chake wa kupiga marufuku mikutano hiyo! Kama msimamo wake ni tofauti na wa chama chake na hivyo serikali, je anafikiri anafaa kuendelea kuhudumu katika ofisi yake?

Iko wapi ile kanuni ya uwajibikaji wa pamoja? Ahhh Nape tupumzishe kidogo.

Wachina waongeza umasikini

Na Tryruckia MFINANGA

BILIONEA Mtanzania na mbunge wa zamani wa Jimbo la Igunga, Rostam Aziz ameonyesha wasiwasi wake kuwepo kwa baadhi ya Wachina walioko Tanzania kwa hadhi ya uwekezaji, kuwa ni wanyonyaji wa wananchi masikini.

Katika kumbukizi ya kujadili namna ya kuenzi urithi wa Maalim Seif Shariff Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, iliyofanyika Jumamosi, Kisiwani Unguja, Rostam alishangaa kuona idadi kubwa ya Watanzania wamekuwa wakishiriki kucheza kamari kwa lengo la kupata utajiri wa harakaharaka – bila kujua njia hiyo ni chanzo kikubwa cha kuchochea kasi ya umasikini.

Tajiri huyo ambaye msimamo wake wa njia ya kupata utajiri ni juhudi, kufanya kazi kwa weledi na uaminifu, amekuwa akisema “hakuna utajiri wa kubahatisha, tena kwa kucheza kamari, bali kwa kujituma.

Rostam ameeleza kutembelea eneo la Mafinga, mkoani Iringa hivi karibuni, ambako alikuta “wawekezaji” kutoka China – wengi wakiwa maeneo ya vijijin, wakiendesha shughuli za kamari.

Amesema Wachina hao hukusanya kiasi kinachokisiwa kufikia Sh. milioni 120 kila mwezi, hali ambayo inaakisi kiasi hicho “kuchotwa” kutoka kwa watu masikini wanaoishi maeneo hayo.

“Nimefika Mafinga, Wachina wanauza simu za mkononi, na wamefungua kasino (maeneo ya kucheza kamari) kwenye vijiji vyetu, kwa sababu watu wetu hawawezi kwamba mwekezaji huyu anapata mapato ya Sh. milioni 120 kila mwezi, ambazo kimsingi ni jasho la watu masikini wa maeneo hayo,” aliongeza.

Rostam anasema mapato hayo maana yake ni kwamba Mchina huyu anafilisi watu wetu masikini kwa kiasi hicho cha fedha, wakati fedha hizo zingetumika kwa shughuli zingine za maendeleo ya familia na hatimaye taifa, badala ya



Rostam Aziz

kucheza kamari.

Pamoja na Rostam kuelezea Mafinga “wawekezaji wa kasino vijijini,” uchunguzi uliofanywa na Pambazuko umebaini kushamiri kwa michezo ya kamari kuwepo mitaani, hasa Dar es Salaam ambako huko watoto wakiwa vinara wa mchezo huo.

Kimsingi, imebainika kwamba mashine nyingi za kamari – maarufu kwa jina la Bonanza, zinamtaka mchezaji acheze kiasi kikubwa cha fedha kwa ushawishi wa kupata zaidi, hatua ambayo ni “ulaghai wa kibiashara.” Kiasi kinachotakiwa kuwekwa kwenye mashine kwa kuanzia ni Sh. 200.

Rostam anaeleza kuwa Tanzania inahitaji wawekezaji makini kwa kuwa milango yenye usalama kwa wenye mitaji mikubwa, imeimarishwa na haiwezi kuvurugwa kwa kuwa walioko madarakani wanaelewa umuhimu wa kuwa na wawekezaji wenye mitaji mikubwa.

Alihimiza serikali kujenga miundombinu yenye kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanashiriki kuimarisha uchumi wa nchi yao kwa kuona na kuchukua fursa zilizopo.

Wachina waongeza umasikini

“Tusipoiarisha uwezo wa watu wetu kushiriki katika uchumi, tutajikuta tunagawana umasikini badala ya kugawana utajiri, kwa kuwa watu wetu hawana elimu na ujuzi, ndiyo maana tunapata wawekezaji uchwara, ambao wanakujia kuchukua fursa za Watanzania, mithili ya mtu anayeona kwa mbali, anangia katika kundi la watu wasioona kabisa, huko anaweza kuwafanyia anavyotaka kwa kuwa hawaoni,” alisema.

Msimamo wa Rostam, unaungana na ule wa mwanahabari na mwanasheria nguli, Jenerali Ulimwengu ambaye amekuwa akieleza kwamba kamari ni utapeli.

Ulimwengu amekuwa akiieleza serikali kuangalia upya suala la uchezaji kamari lililozagaa nchini kwa sababu michezo hiyo ni utapeli, na inasaidia kujenga imani kuwa watu wanaweza kuishi, na kuendesha maisha yao, bila kufanya kazi bali kwa kushinda katika nyumba za kucheza kamari.

“Watu wanadanganywa kupoteza pesa kidogo waliyonayo katika shughuli isiyoweza kuzalisha...ni uongo mkubwa, ni matapeli wakubwa hawa, wanadanganya vijana wetu...redio za FM na viduka vya ‘betting’ ndiyo yamekuwa maisha ya vijana wetu...”

“... Serikali inahangaika kutoa elimu, na watoto wanayo hamu ya kupata

elimu, lakini wakikua kidogo tu, wanaaza kupumbazwa kwa kudanganywa kuwa wanaweza kupata pesa na kutajirika bila kufanya kazi,” anaongeza.

Akimzungumzia Maalim Seif (sasa marehemu), Rostam alitanabaisha kwamba haiba ya kiongozi huyo ni nadra kupatikana mara kwa mara, kwani maono yake na namna alivyokuwa akiipenda nchi yake, bila unafiki – ni wa kipekee.

“Maalim ni mtu aliyejitoa nafsi yake na akaukataa ubinafsi kwa kujali nchi yake na watu wake. Huyo ndiye Maalim Seif. Ni aina ya viongozi ambao ni nadra sana kutokea katika nchi. Huwa ni zawadi kutoka kwa Mungu na huchukua miaka mingi na vizazi kadhaa kabla ya kuja mwengine,” aliongeza Rostam.

Akizungumzia kuwepo kwa fursa kubwa hivi sasa kwa wawekezaji makini, Rostam amesema kuwa tangu ameingia madarakani Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, wamekuwa mstari wa mbele kushawishi mitaji kutoka nje kuingia nchini kwa imani kwamba mitaji ya wawekezaji italindwa.

Katika kipindi cha mwaka mmoja tangu Machi 2021 mpaka Machi 2022, mitaji kutoka nje iliyoingia Tanzania iliongezeka kwa asilimia 300 kutoka dola za Marekani

Endelea Uk. 7



Kasino

Wachina waongeza umasikini

1.13 bilioni mpaka 4.144 bilioni.

Rostam anasema kuwa uwekezaji wa kiwango hicho – ambacho kimekuwa kikiongezeka kwa kasi, hautakuwa na tija kubwa, iwapo Watanzania hawataandaliwa kuwa na elimu yenye ujuzi na weledi kuweza kunufaika.

Alieleza kuwa Maalim Seif alitaka kujenga Zanzibar yenye watu wenye elimu na maarifa ya kutosha kuendesha uchumi ambao unatoa huduma kwa eneo lote la Afrika Mashariki, Maziwa Makuu na Bahari ya Hindi.

“Kuiishi dira yake, tunapaswa kujielekeza huko na hiyo itakuwa njia nzuri zaidi na namna bora kabisa ya kumuenzi Maalim Seif ambaye watu wengi bado wanakumbuka maono yake kuhusu Zanzibar na watu wake,” alisisitiza Rostam.

“Juhudi zinazofanyika sasa za Rais Mwinyi kutazama sekta ya elimu Zanzibar na kutoa mwanya kwa wataalamu kufanya tathmini ili kupata njia za kuboresha zaidi kuendana na wakati wa sasa wa teknolojia na uwekezaji makini, lazima zipongezwe na kuungwa mkono,” alisema Rostam.

Anasema kwa kukuza elimu na kuweka fursa kwa Wazanzibari wengi zaidi kunufaika na uwekezaji, ni njia nzuri zaidi ya kuenzi mchango wa Maalim Seif.

“Lakini kama nilivyosema, elimu bila ya umoja na maridhiano miongoni mwa Wazanzibari haitotufikisha popote. Bahati nzuri, kwa jinsi ninavyomfahamu Dkt. Hussein Mwinyi ni muumini wa maridhiano, na kwa kuwa anajali maendeleo ya Wazanzibari na kwa sababu anajua hayawezi kupatikana bila maridhiano, basi naamini tutaona maridhiano yanaimarika zaidi,” alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abraham Kinana akimzungumzia Maalim Seif, alisema ni kiongozi aliyekuwa na sifa nyingi nzuri zinazomfanya kuwa mtu mwenye maono, msimamo, subira, mpenda haki,



Mfano wa Fedha taslim za Tanzania

mwanamapinduzi na mwenye ushawishi.

Alisema Maalim alipenda kuona vijana wanapata elimu bora iliyolingana na mahitaji ya wakati na yenye kuwajenga vijana kudadisi, kujituma, kujitegemea na kuwa wazalendo kwa nchi yao.

Kinana alisema Maalim Seif aliamini kwa dhati kuwa elimu ndiyo mkombozi wa kweli kwa mwanadamu, ndio maana elimu yake ya msingi na ya juu alipata kwa kujituma bila kukata tamaa.

“Jukumu hilo lilikuwa zito kwa kuwa fursa za elimu zilikuwa ndogo na hafifu, kwa ujasiri mkubwa na kwa hatua za kuthubutu alijitwisha dhamana ya kufanya kazi aliyopewa kwa ustadi, hamasa na ari kubwa,” alisema.

Alieleza kuwa, kutokana na juhudi zake, vijana wengi wa Zanzibar walipata nafasi za elimu ndani na nje ya nchi, ambapo Maalim aliamini katika elimu, nafasi ya elimu na fursa zinazotolewa na elimu katika maisha ya binadamu na uhai wa taifa.

Huu ni mwaka wa pili sasa kunakuwepo na makongamano ya kumkumbuka Maalim Seif aliyefariki dunia Februari 17, 2021 baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Kutenda zaidi ya sheria na katiba

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

NILIPOZUNGUMZIA juu ya mwenye mamlaka ya kugawa madaraka niligusia jambo la katiba. Nilisema kwamba katiba ndio sheria ya msingi inayolinda mkataba wa utawala katika taifa.

Katiba ni mwongozo wa msingi ambao wenye nchi huwapa wale wanaowakabidhi dhamaana ya kuongoza taifa. Mkataba huu hauachi nje kundi lolote la watu wowote. Humo hutamkwa wajibu wa kila kundi katika jamii ya kisiasa pamoja na haki zao. Kwa uelewa huo hakuna yeyote aliye juu au chini; zaidi au pungufu ya matakwa ya katiba ya nchi.


Upo usemi na umekuwa ni uzoefu kwamba madaraka ni uharibu nafsi (corrupt). Mara nyingine watu wanapoingia katika madaraka hutamani kujilimbikizia nguvu zaidi. Kwa hali hiyo ili kujipa nguvu hizo hutokea kwamba katiba na sheria hukiukwa.

Katika kufanya hivyo ndipo watawala huanza kuingia katika kutoa matamko ambayo ni kinyume na katiba na sheria na kutafuta washabiki ambao watatetea uasi huo. Huu ni mzunguko wa kawaida katika safari ya kuelekea utawala wa kidikteta.

Wakati kwingine twaweza kusema kwamba maadui wakubwa wa utawala wa sheria ni mashabiki wa watawala wanaovunja katiba na sheria na kujiweka juu ya hizo. Hawa ni hatari kuliko hata hao watawala wenyewe kwa sababu ni hao wanaowapa nguvu za kufanya hivyo.

Madikteta wengine wasingefika mbali iwapo wasingekuwepo watu wa kuwapigia tarumbeta na hata kuangamiza wale wote wanaothubutu kupinga. Katika kila udikteta kuna wanufaika ambao huulinda udikteta huo kwa gharama zozote.

Zipo njia nyingi za kupoka watu nguvu zao za kisiasa na kuziwekeza nguvu hizo kwa watawala. Hili hufanyika kiurahisi



Katiba

hasa katika mataifa ambayo ni machanga katika utawala wa demokrasia. Njia mojawapo ya jinsi ya hili kufanyika ni katika lugha za kutukuza watawala zilizo kinyume na uwiano wa madaraka uliomo katika katiba. Kwa mfano upotoshaji juu ya umiliki wa mali za taifa.

Mara kadhaa wapo wanaotaka kuaminisha jamii kwamba fedha zinazokusanywa pamoja na raslimali za mataifa yao ni za watawala. Hivyo kutaka kuonyesha kwamba miradi yote ya maendeleo inayofanyika ni kwa hisani za watawala.

Huu ni upotoshaji pale ambapo katiba haitoi nguvu za jinsi hiyo kwa mtawala. Itoshe kuelewa jinsi katiba na sheria zinavyosema juu ya mambo kama hayo na itoshe kusema na kufanya kwa kiwango kile ambacho katiba na sheria zinasema juu ya jambo husika.

Zipo njia nyingi za kuvunja sheria ambapo mojawapo ni hiyo tuliyotaja hapo juu. Udikteta sio tu kutawala pasi kufuata sheria bali ni pamoja na watawala kuchukua nafasi ya sheria. Hatari zaidi ni pale umma unapoaminishwa kwamba watawala ndio wenye neno la mwisho hata kama neno hilo ni kinyume cha sheria.

Hii ndio sababu ni muhimu sana kuwepo na mpango mahsusi wa elimu ya uraia kwa wananchi. Katika mataifa ya kidemokrasia na ya wakereketwa wa utawala wa sheria ni muhimu watu waelewe vitu kama vile katiba ya nchi na sheria zingine za msingi.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Tunalea uzembe hadi lini?

MIONGONI mwa changamoto zinazokwamisha maendeleo yetu ni kuwepo kwa baadhi ya watendaji wa serikali wasiotekeleza majukumu yao ipasavyo.

Licha ya changamoto hiyo kuchelewesha au hata kukwamisha maendeleo katika maeneo mbalimbali, watendaji wengi wamekuwa wakibainika kufanya ufsadi, kwani wanalipwa mishahara bila kutekeleza wajibu wao kiutendaji.

Kuna matukio mawili ya hivi karibuni yanayothibitisha uwepo wa changamoto hiyo.

Katika tukio la kwanza, majuzi Oktoba 14 katika kilele cha mbio za mwenge kwenye Uwanja wa Kaitaba, mkoani Kagera, Rais Samia Suluhu alisema “si sahihi taarifa za rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma zijirudie kila mwaka katika ripoti za kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru na ripoti ya Mdhidhi na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) huku kukiwa na vyombo na taasisi zenye dhamana ya kudhibiti vitendo haziriyo.”

Rais alitoa maagizo kwa Taasisi ya Kupambana na Kuzuwia Rushwa (Takukuru) na ile ya Zanzibar (ZAECA) kuchukua hatua stahili. Na hapo ndipo kwenye chanzo cha tatizo. Kwanini Takukuru na ZAECA zisubiri maagizo ya Rais badala ya taasisi hizo kutimiza wajibu wao ipasavyo?

Katika tukio la pili, Oktoba 18 iliripotiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alikagua ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Namtumbo na kutoridhishwa na “utendaji wa ovyo.” Waziri Mkuu alinukuliwa akisema, “nimekagua ujenzi wa hospitali ya wilaya lakini, sijaridhishwa na hali ya ujenzi, nimeagiza milango yenye hitilafu yote ing’olewe na iwekwe yenye hadhi ya hospitali ya wilaya, iweje iwe imeacha nafasi juu hadi



Rais Samia Suluhu Hassan

vidole vinapita?”

Unaweza kujiuliza, hivi mkoa wa Ruvuma hauna Mkuu wa Mkoa? Au je Wilaya ya Namtumbo haina Mkuu wa Wilaya? Vipi kuhusu Katibu Tawala wa Mkoa na Katibu Tawala wa Wilaya? Vipi kuhusu Mhandisi wa Mkoa na wilaya?

Maana kama viongozi hao wapo, iweje basi hadi Waziri Mkuu atembelee ujenzi wa hospitali hiyo ndipo zibainike kasoro zilizotajwa?

Kama ilivyokuwa kwenye ubadhirifu wa fedha za miradi ya mwenge ambao ulibainishwa na Rais Samia, mapungufu hayo katika ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Namtumbo yaliyobainishwa na Waziri Mkuu Majaliwa ni matokeo ya uwepo wa watendaji wasiotimiza wajibu wao ipasavyo.

Mwisho, changamoto hiyo itaendelea kuwepo endapo wahusika wataishia kukumbushwa tu wajibu wao badala ya kuchukuliwa hatua.

Wizi wa kutisha Pride

Na Waandishi WETU

KAMPUNI ya Serikali ya Tanzania, Kitwayo Pride ni sawa na “shamba la bibi” kwa watendaji wake kuigeuza mali binafsi kwa kuchota mabilioni ya fedha kama wanavyotaka.

Watendaji hao, mbali na kuchota mabilioni ya fedha kwa faida binafsi na pengine kugawana rasilimali za kampuni hiyo na baadhi ya wakubwa serikalini, walianza mbinu chafu za kuipoka kutoka kwenye umiliki wa serikali ili kuwa mali binafsi.

Pambazuko limebaini pasinashaka kwamba watendaji wakuu wa Pride walikuwa “wakihomola” kiasi kikubwa cha fedha bila woga, huku wakitamba kwamba “hakuna wa kuwatisha” – kwani walikuwa wamewaweka mifukoni mwa wanaowataja kuwa “wakubwa serikalini.”

Gazeti hili limebaini kuwa kuna uwezekano mkubwa kwamba baadhi ya viongozi wa juu wa Pride kwa kushirikiana na “wakubwa” wamehamisha kiasi kinachofikia Sh. bilioni 1.8 kutoka akaunti za kampuni hiyo na sehemu kubwa ya fedha hizo imehamishiwa nje ya nchi.

Kutokana na wizi na ubadhirifu ndani ya Pride, ofisi zald nyingi hasa za pembezoni mwa Dar es Salaan na mikoani zimefungwa – na zile zinazooneka kuwa na milango mibovu, zikigeuka makazi ya popo na wadudu kama buibui.

Ni kwa sababu hiyo, watendaji wake lukuki – hasa wale wenye nafasi za chini, wako majumbani wakisubiri “neema ya serikali” kuifufua huku hatma ya madai yao ikishindwa kujulikana.

Hali mbaya ya fedha ya Pride inaifanya kampuni hiyo kutokuwa na majukumu yanayoendelea Pride licha ya kwamba hivi karibuni, Julai 28, 2022, Rais Samia Suluhu Hassan, alimteua Sarah Kinyamfura Barabomoka, ambaye ni Mwandishi Mkuu wa Sheria Mstaafu, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi.



Waziri wa Fedha na Mipango Mwigulu Nchemba

Pride ambayo kimsingi ilianzishwa ili kuwa msimamizi wa fedha na maendeleo ya vijijini, ikageuka kunufaisha wakubwa na matajiri badala ya walengwa. Fedha ya awali (mtaji) ilitolewa na Serikali ya Norway.

Pride ni kifupisho cha maneno ya Kiingereza ambayo ni - Promotion of Rural Initiatives and Development Enterprises.

Lakini, hadi sasa Barabomoka hajaanza kazi na huenda asiwe na kazi yoyote ya kufanya ndani ya Pride kwa sababu ya hali mbaya ya kifedha inayoikabili Pride kwa sababu ya ubadhirifu wa mali na fedha, mzigo mkubwa wa madeni na udanganyifu katika malipo yanayofanywa.

Ubadhirifu wa mali na fedha

Kulingana na Taarifa ya Mwaka 2018/19, iliyosainiwa na Mkgazuzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali

Inaendelea Uk. 11

Wizi wa kutisha Pride

Inatoka Uk. 10

(CAG), Charles Kicheere inaeleza kuwa uongozi wa Pride ulikuwa ukifanya malipo ya kitapeli pamoja na ufujaji wa mali na fedha za kampuni.

Kuhusu ufujaji wa mali na fedha za kampuni, CAG anasema kuwa, hadi Oktoba 31, 2019 - Pride ilikuwa na jumla ya mali zenye thamani ya Sh. bilioni 19.97. Mali hizi zilijumuisha Sh. bilioni 8.82 kama mikopo kwa wateja; na Sh. bilioni 11.14 kama mikopo ya motisha kwa wafanyakazi.

Mikopo ya wafanyakazi ilikuwa katika makundi matatu: mikopo ya nyumba, mikopo maalum, na mikopo ya jumla.

Kati ya mikopo ya Sh. bilioni 11.14 kwa wafanyakazi, Sh. 745.59 milioni ni mikopo kwa wafanyakazi 168 ambao walikuwa wameacha kufanya marejesho na hakukuwa na hatua zozote za kiutawala kuwataka warejesho mikopo husika; Sh. 10.38 bilioni ni mikopo ya waajiriwa 33 ambao walikuwa hawajaanza kufanya marejesho; na Sh. 2.6 bilioni ni mikopo kwa waajiriwa wasiojulikana.

Pambazuko linatambua kuwa hadi kufikia Juni 30, 2020, hakuona kumbukumbu zozote zenye kuonyesha ukamilifu wa mali za kampuni, wala madeni yaliyokusanywa, wala kumbukumbu zenye kuonyesha kwamba madeni yanaendelea kudaiwa.

Gazeti hili limeona taarifa zinazoonyesha kuwa taarifa ya ukaguzi wa hesabu ya Desemba 31, 2016, kampuni ya Pride ilikuwa inamiliki mali kadhaa ambazo, hata hivyo hazikutajwa kwenye orodha ya mali ya kampuni ya Oktoba 31, 2019, na hakuna maelezo zimekwenda wapi.

Mali ambazo hazionekani, ni pamoja na hisa zenye thamani ya Sh. bilioni 2.31 zilizokuwa zimewekezwa ndani ya Benki M; bilioni Sh. 48.20 zilizokuwa zimetunzwa kwenye akaunti za kuweka akiba katika benki zingine za ndani; ardhi zenye thamani ya Sh. bilioni 1.44; na mali nyingine.

Kwa sababu ya makosa haya, CAG alipendekeza kwamba, wahusika wote, wakiwemo waajiriwa na menejimenti, wachukuliwe hatua za kisheria, kwa sababu ya kujihusisha na ubadhirifu wa mali na fedha za kampuni. Pia alipendekeza kwamba, ateuliwe mthamini wa mali za serikali kwa ajili ya kuchunguza wapi zipo mali za kampuni ambazo hazionekani.

Mzigo mkubwa wa madeni

Pambazuko limeleza kuwa Pride imekuwa na mzigo mkubwa wa madeni yanayofikia Sh. bilioni 130.11, yenye mchanganuo ufuatao: Madeni yanayohusiana na mikopo ya benki za ndani (bilioni 29.9); Madeni yanayohusiana na benki za nje (bilioni 59.8); tozo na makato yanayohusiana na taasisi za kiserikali (bilioni 19.11); Madeni yanayohusiana na watoaji wa huduma kwa Pride (bilioni 2.02); Madeni yanayohusiana na bima ya afya (bilioni 0.887); Madeni yanayohusiana na amana za wateja waliokuwa wameomba mikopo (bilioni 8.27); Madeni yanayohusiana na mishahara ya waajiriwa (bilioni 5.89); na madeni yanayohusiana na amana za makato ya watumishi kupitia 'sakosi' ya watumishi wa Pride iitwayo Fahari yetu (bilioni 4.95).

Udanganyifu katika malipo

Imefahamika kuwa ndani ya Pride tangu Januari 1, 2017 hadi Oktoba 31, 2019, amebainika kuwa Sh. bilioni 4.53 zililipwa nje ya utaratibu rasmi wa kudhibiti na kusimamia malipo ya kampuni hiyo. Malipo ya Sh. bilioni 4.53 hayakuidhinishwa, hayakuwa na viambatanisho sahihi, na yalifanyika kwa kutumia njia ya udanganyifu.

Kwa mujibu wa mfumo wa kanuni za kuratibu malipo ndani ya Pride, malipo yote yanapaswa kuanzia kwa mleta maombi, kuthibitishwa na mkuu wa idara ya mleta maombi, kuhakikiwa na wahasibu wa idara ya fedha, na hatimaye

Wizi wa kutisha Pride

kuruhusiwa na meneja wa fedha Pamoja na mkurugenzi mtendaji.

Gazeti hili limegundua kuwepo kwa udanganyifu katika maeneo yafuatayo; malipo yasiyo na sahihi, fomu ya maombi, wala jina la mhasibu aliyeyachakata (milioni 660.73); malipo yasiyo na viambatanishi vya kiushahidi (milioni 1,687); malipo yasiyo na uhalali yaliyolipwa kwa watendaji na wajumbe wa bodi (milioni 139.43); malipo yaliyofanyika bila kuonyesha lengo wala kazi husika (milioni 508,37).

Malipo mengine ni kupitia kwenye matawi ya Pride kwenda kwa wapokeaji wasiojulikana kwa msaada wa miamala ya fedha za kielektroniki inayofanyika kwa kutumia simu za mikononi (milioni 405.47); malipo ya fedha taslimu kwa wadai hewa, kwa maana ya watu ambao hawakutoa huduma zozote kwa Pride (milioni 585.93); na matumizi ya nyaraka feki na majina bandia kutoa mikopo kwa stafu (milioni 540.96).

Kuna kila dalili kwamba malipo haya yalifanywa ili kunufaisha baadhi ya watendaji wa Pride wenye kuhusudu wizi, ubadhirifu na kukosa uaminifu kwa mwajiri wao, pia kuwepo kwa mifumo dhaifu ya udhibiti wa kifedha.

Watanzania wengi wamekuwa wakilalamikia namna Pride ilivyokuwa ikifanya kazi ikiwamo “kunyanyasa” baadhi ya wateja wake, hasa wanawake wanapochelewa kurejesha mikopo yao “kiduchu.”

“Kama ambavyo mashirika mengi ya serikali yamekuwa kichaka cha wizi, Pride nayo ni mfano mwingine wa hovywa kupotea kwa fedha za serikali na kuminywa kwa fursa za kutokomeza umasikini kwa Watanzania,” anasema Dkt. Lenny Kasoga alipotoa maoni yake kuhusu hali ya fedha ya Pride.

Mgogoro wa umiliki wa Pride

Kihistoria, Pride ni kampuni iliyooanzishwa Mei 5, 1993 kwa ajili ya kukuza maendeleo ya vijijini kwa njia ya kuanzisha na kuhami kifedha miradi ya



Jengo la Benki Kuu ya Tanzania

vijijini. Waanzilishi ni Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Norway.

Lakini, tangu mwaka 2016, kulizuka mgogoro kati ya serikali na wakurugenzi wa Bodi ya Pride kuhusu umiliki wa Pride. Kesi namba 130 ya mwaka 2016 ilisajiliwa Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara, na kuanza mbele ya Jaji B. K. Phillip.

Walalamikaji walikuwa ni wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Pride, wakiwakilishwa na Wakili Michael Kamba. Waliomba Mahakama kutamka kwamba “Pride ni kampuni inayomilikiwa na Bodi ya Wakurugenzi kwa asilimia 100.” Walalamikiwa walikuwa ni Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, iliomba Mahakama Kuu kutamka kwamba Pride ni kampuni inayomilikiwa na Serikali ya Tanzania na serikali ina maslahi katika kampuni kwa asilimia 100. Hukumu ya kesi hii ilisomwa Oktoba 18, 2018 na maombi ya serikali kuthibitishwa kisheria.

Mara tu baada ya hukumu huu kusomwa, Julai 4, 2019, Wizara ya Fedha na Takukuru walikubaliana kwamba Ofisi ya CAG ifanye ukaguzi kwa ajili ya kupima uhimilivu wa kifedha ya kampuni ya Pride tangu mwaka 2016 mgogoro wa kisheria ulipozuka hadi Oktoba 31, 2019.

Kiswahili hakina dereva, wote abiria

Na Shabaan LULELA

MWALIMU Julius Nyerere aliwahi kueleza kuwa taifa lisilojivunia lugha yake halina uhai, lakini pia Wachina wakaenda mbali kidogo kwa kusema nchi isiyotumia lugha yake kujitea maendeleo makubwa - kwanza ya wananchi wake na baadaye ya wengine, ni sawa na maji yaliyooshewa maiti.

Kwamba maji yakiohewa maiti yanakosa faida kubwa inayoweza kuelezwa. Yakitumika, basi yametumika.

Wachina kama ilivyo kwa Mwalimu Nyerere (sasa marehemu) wote wana maana kubwa katika dunia ya sasa inayohitaji mwenye nguvu au anayetumia ubunifu zaidi kuhakikisha maendeleo makubwa na ya haraka ya familia na taifa yanapatikana.

Kwa kiasi kikubwa, dhana ya Mwalimu Nyerere imejikita mno Tanzania na watu wake wameielewa na wameendelea kujivunia lugha ya Kiswahili. Lugha hiyo, mbali na kuwaunganisha wananchi kupigania uhuru wao na baadaye maendeleo yao, bado haijaweza kumea na haina mizizi ya kuhakikisha inakuwa rasilimali nyingine kubwa ya kuingiza fedha kwa wananchi na hata katika Hazina ya Tanzania.

Hali hiyo ya kushindwa kukisambaza Kiswahili na kukifanya mtaji wa kuleta fedha nyingi kutoka nje ya nchini, kunatufanya tusiwe mbali sana na falsafa ya Kichina kwamba lugha yetu, mbali na faida kidogo inayopatikana, hakuna anayeipigania ili iwe mtaji.

Kila mmoja wetu; iwe serikali yenyewe, taasisi zake, mashirika, watu binafsi na hasa wasomi, anajipiga kifua tu ndani ya maeneo ya nchi yetu mbele ya umati akipiga 'kelele' za kuhimiza ukuzaji wa Kiswahili, lakini juhudi za kukigeuza fedha hazionekani.

Wapo waliopanda majukwaani, tena wakizungumza na povu likiwatoka midomoni mwao; kwamba Kiswahili lazima kipiganiwe kwa nguvu zote ili



Mwl. Julius Nyerere

kuhakikisha kinapasua anga na kuwafikia watu wengi zaidi nje ya nchi.

Hao walifanya hivyo kwa nia njema kabisa, lakini nguvu zao zinakatishwa na Waswahili wenzao, tena ajabu Watanzania wakidai lugha hiyo haina lolote na wala siyo chochote nje ya mipaka ya Tanzania. Hawa baadhi yao ni wasomi, waandishi wa habari na hata viongozi wa siasa.

Kukatishwa kwao tamaa na ndugu zao kukawavunja moyo na wakaamua kuacha na kuendelea na shughuli zao.

Wenzetu Wakenya, ambao historia inawataja kuwa 'wanafunzi' wetu katika lugha, wao wanaonekana kuwa walimu zaidi katika taasisi na vyo vya nje, tena wakitengeza fedha nyingi.

Kama ilivyo katika utalii, Wakenya ndiyo wanaotangaza kuwa magwiji wa Kiswahili na kwamba ni lugha inayokuwa na kuzungumzwa na idadi kubwa ya Waafrika. Katika matangazo yao wanasema; -unataka kufanya kazi au biashara Afrika, basi jua kuzungumza lugha ya Afrika- Kiswahili.

Sisi inavyoonekana jitihada zetu zimo ndani ya nchi tu. Tumelala. Tunaonekana mno katika vipindi vya televisheni tukikizungumza na kukichambua Kiswahili, lakini nguvu ya kukitangaza na kukipeleka nje haionekani.

Ng'ambo ni asali ama shubiri -2?**Na Godwin CHILEWA**

WIKI iliyopita tuliona namna yaliyvo maisha ya Watanzania ambao wanaishi na kufanya shughuli zao Marekani, au ughaibuni kwingine kokote.

Tuliona jinsi fursa zilizopo na kwa kiasi gani zinaweza kugeuka kuwa kitu cha msaada kwa mhusika na familia yake au kuwa laana kutegemea na mtu mwenyewe.

Jiulize kitu gani kilichofanya maisha ya wengi wa 'wabeba boksi' wa ughaibuni kubadilika kiasi cha kuweza kuishi maisha ya kifahari, kufanya miradi mikubwa nchini Tanzania, na hata kuanza kuheshimiwa kiasi cha kuitwa wawekezaji?

Jibu ni kwamba katika kipindi cha miaka kumi na tano hivi na kuendelea, asilimia kubwa ya Watanzania walioko nje walifanya mikakati imara ya kuboresha maisha yao hatua kwa hatua.

Kwanza walitafuta vibali vya kuwaruhusu kuishi katika nchi walizopo kihalali na hivyo kufungua fursa za kufanya kazi za maana. Hii ni hatua ya msingi sana kwa kila mwana-diaspora, kwani bila ya vibali vya ukaazi, siyo rahisi kupata kazi nzuri au kuishi maisha ya uhakika.

Jambo la pili vijana hawa walizingatia umuhimu wa kuwekeza kwenye elimu. Asilimia kubwa ya vijana baada ya kupata vibali vya ukaazi, walijikita kusomea fani mbalimbali zilizowawezesha kupata ajira za maana na za kudumu.

Wengi walisomea taaluma ya huduma za afya na kuhitimu kuwa wauguzi au wafamasia. Wengine walijikita katika sayansi na teknolojia (IT), uongozi, biashara na fani nyinginezo. Hatua hii imesaidia sana kuinua kipato cha watanzania wengi kwa asilimia kubwa mno.

Kwa mfano, muuguzi wa kawaida (Registered Nurse) katika majimbo mengi analipwa kati ya dola 30 hadi 45 kwa kila saa anayofanya kazi. Kwa lugha rahisi,

**Muuguzi**

muuguzi anayefanya saa nane kila siku kwa wiki moja, anaweza kutengeneza kati ya dola 1,200 hadi dola 1,800 sawa na Sh. 2,760,000 hadi 4,140,000 kwa wiki.

Wauguzi mabingwa na vijana wataalamu wa IT, wanafikisha hadi Sh. milioni 12 kwa wiki, kutegemea pia kampuni anayoitumikia.

Wapo pia vijana wengi waliojiajiri na au kufungua kampuni za usafi, ubunifu wa mavazi na mitindo, usafirishaji, maduka ya bidhaa kutoka Afrika, na biashara nyingine za aina mbalimbali.

Kwa ujumla ingawa bado hatujawa na mamilionea wa Tanzania wanaoishi Marekani wengi wanaojulikana, lakini wapo vijana wengi waliojiimarisha vyema kiuchumi.

Haya yote yamewezekana kwa sababu mfumo wa siasa, sheria na uchumi wa Marekani unampa fursa kila mtu kusonga mbele kiuchumi.

Jambo pekee analopaswa kufanya ni kuwa mbunifu, mwenye juhudi, na mwenye kuzingatia sheria na taratibu. Hili ndilo linalofanya Marekani kuitwa nchi ya fursa (The land of opportunity).

Mwandishi wa safu hii ni Mtanzania anayeishi na kufanya shughuli zake Texas, Marekani.

Hujambo

Ukanushi katika njeo iliyopita

Na Dkt. Michael Mashauri

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo tutakuwa na darasa juu ya kiambishi cha ukanushi katika njeo iliyopita (**Negation in Past Tense**) ni **Ha-** kinachofuatiwa na kiambishi cha nafsi isipokuwa nafsi ya kwanza umoja inayotumia **si-** na hudondosha kiambishi

cha nafsi.

Baada ya kiambishi na nafsi hufuatiwa na kiambishi **-ku-** kabla ya mziwi wa kitenzi. Nafsi ya pili umoja inaweza kutumia **hau-** au **hu-** na nafsi ya tatu umoja hudondosha kiambishi cha nafsi **-a**.

(Prefix for negation in past tense is **Ha-** which is followed by the personal prefix (or object prefix) except for first person singular which uses **si-** and drops the personal prefix.

After personal prefix, it is followed by the prefix **-ku-** before the verb root. The second person singular can use **hau-** or **hu-** and the third person singular drops the personal prefix **a-**.)

Examples			
1 st Person	Singular	Affirmative	Niliwinda wanyama (I hunted animals)
		Negative	Siku winda wanyama (I didn't hunt animals)
	Plural	Affirmative	Tulienda shuleni (We went to school)
		Negative	Hatuku enda shuleni (We didn't go to school)
2 nd Person	Singular	Affirmative	Wewe ulicheka (You laughed)
		Negative	Wewe hukuche ka (You didn't laugh)
		Negative	Wewe haukuche ka (You didn't laugh)
	Plural	Affirmative	Nyinyi mlilia (You are cried)
Negative		Nyinyi hamkul ia (You did not cry)	
3 rd Person	Singular	Affirmative	Yeye alifuraha kula ugali (He/she enjoyed eating ugali)
		Negative	Yeye hakufur ahia kula ugali (He/she did not enjoy eating ugali)
	Plural	Affirmative	Wao walilala hapa (They slept here)
		Negative	Wao hawakul ala hapa (They didn't sleep here)

Kwa nomino za ngeli nyingine, ukanushi hujitokeza kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini. (For nouns from other noun classes, negation appears as shown in the table below.)

Examples			
Singular	Affirmative	Kiti kilivunjika (A chair broke)	
	Negative	Kiti hakiku vunjika (A chair was not broken)	
Plural	Affirmative	Viti vilivunjika (chairs broke)	
	Negative	Viti haviku vunjika (chairs did not break)	

• Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Alibakwa na kuambukizwa Ukimwi, lakini sasa shujaa

Ni binti anayetimiza miaka 30 mwaka huu. Alibakwa akiwa na miaka 10 na kuwa chanzo cha kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Ameishi na virusi vya ugonjwa huo kwa miaka 18 na sasa anapigania ustawi wa watu wengine ili wasiupate na wale walioambukizwa; waishi bila hofu ya kifo. Makala haya ya mahojiano na Niqita Pieterse anayeishi Durban, Afrika Kusini, yameandikwa na Simon Mkina wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa), yanaeleza zaidi...

Swali: *Mara nyingi umejitambulisha kuwa shujaa wa vita dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi, kwanini umeamua kujitangaza jemedari?*

Jibu: Ama hakika mimi ni jemedari, unaona hata wewe umejua hilo! (anacheka). Vita nimevishinda, kwanza nikiwa peke yangu na sasa naendelea kukusanya jeshi kubwa ili ushindi uwe mkubwa zaidi na siku moja sote tufurahie ushindi kwa pamoja.

Najiita jemedari, lakini wengine wananiita Malkia wa Ukimwi, haya yote ni majina yangu kuonyesha namna jitihada zangu za kueneza elimu dhidi ya Ukimwi zinavyoshika kasi kila siku.

Swali: *Unakusanyaje jeshi lako na kina nani wapiganaji?*

Jibu: Ushindi dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi unahitaji nguvu ya pamoja, nimeamua kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuelimisha watu, siyo wa hapa Durban, au Afrika Kusini pekee, bali Afrika na dunia nzima.

Jeshi ninalozingumzia hapa ni wale watu walioathirika na kuathirika kwa VVU (Virusi Vinavyosababisha Ukimwi) na Ukimwi na wale ambao wana nia njema kuangamiza ugonjwa huu. Nashukuru nchi nyingi sasa, hasa za Afrika zinatambua juhudi zangu na napokea misaada mingi ya kunipa moyo ili juhudi za kuelimisha jamii ziendelee.

Swali: *Ushindi upi unaozungumzia hapa?*

Jibu: Nazungumzia ushindi dhidi ya VVU vinavyoleta ugonjwa wa Ukimwi. Huu ni ugonjwa usiobagua, unatuathiri



Niqita Pieterse

wote; matajiri kwa masikini, haujali rangi; unashambulia weusi na wazungu wala hauangalii kimo; uwe mrefu ama mfupi, unaweza kuambuzwa tu.

Inaeleweka sasa kwamba Ukimwi unasambazwa kwa njia nyingi, ingawa kubwa na ambayo inafahamika kwa wengi ni njia ya ngono zisizokuwa salama. Njia nyingine ni pamoja na kuchangia vitu vyenye ncha kali na mtu aliyeambukizwa tayari na hata kuongezwa damu ya muathirika.

Katika hilo la ngono zisizokuwa salama, wapo wanaobakwa na wale wanaoamua kutotumia kinga dhidi ya

Alibakwa na kuambukizwa Ukimwi

Ukimwi. Kinga salama zaidi ni kutumia kondomu.

Swali: Wewe lipi lilikukuta hata ukajikuta umembukizwa Ukimwi?

Jibu: Mimi nilibakwa nikiwa na miaka 10, wakati huo binti mdogo kabisa nikiwa bado nasoma elimu ya msingi. Nilifanyiwa ukatili huo na baba yangu mdogo ambaye alikuwa anaishi kwenye familia yetu. Ni mtu ambaye aliaminika na kuthamaniwa sana pale nyumbani, lakini kumbe alikuwa mtu mbaya sana asiyekuwa na maadili ya kijamii na kimila.

Pamoja na kuwa baba mdogo, lakini pia alikuwa rafiki yangu mkubwa, kila mara, baada ya masomo alikuwa akinifundisha hesabu na masomo mengine, siku za wikiendi alinichukua kwenda matembezi na kuninunulia vitu vidogo vidogo madukani.

Hakuwahi hata siku moja kuniambia ananitamani kwa mtazamo wa kingono. Nami sikuwa na mawazo mabaya juu yake. Lakini mwisho wa siku alinigeuka na kunibaka tukiwa ndani ya nyumba yetu. Ilikuwa siku ya Jumamosi ambapo hapakuwepo watu ndani, walienda matembezini. Yeye aliamua kubaki na kunishawishi kubaki naye tukiangalia vipindi vya televiseni.

Swali: Alikushawishi kwa lipi?

Jibu: Tukiwa tumeketi tunaangalia televisheni, alianza kunishikashika, nami sikupenda na nilimwambia kuwa sipendi. Lakini aliendelea. Nilimwambia nitamsema kwa mama endapo akiendelea. Aliamua kutumia nguvu kuniingilia kimwili.

Swali: Je, ulipiga kelele ili kumuogofya?

Jibu: Nilijaribu kupiga kelele lakini sikufanikiwa kwa vile alikuwa ameniziba mdomo kwa kiganja cha mkono wakati ananiingilia kwa nguvu. Hakika aliniimiza sana katika viungo vyangu vya kijinsi na baada ya tukio lile nilishindwa kutembea kwa sababu ya maumivu.

Swali: Baada ya wazazi kurejea, uliwaeleza kilichotokea?



Jibu: Ilibidi kuwaeleza wanafamilia. Kilitishwa kikao cha ukoo. Baada ya kuona kikao kimeitishwa, baba mdogo aliamua kukimbia na kutokomea kusikojulikana.

Katika kikao kile, kulitokea minyukano na mtafaruku mkubwa kuhusu kwenda kuripoti kituo cha polisi, wapo waliotaka nikashtaki na wengine wakisema ni aibu kwa ukoo, lakini kwa kuwa tamaduni nyingi za Afrika zinakumbatia mfumo dume - unaoshabikia ukatili wa jinsia, hatukuweza kwenda polisi kushtaki.

Nguvu ya mama na wengine waliokuwa wakitaka twende kushtaki ilishindwa na ile ya wanaume ambao wakiheria na kimaadili, kwenda mbele ya vyombo vya sheria.

Swali: Pole sana, lini sasa uligundua kuwa umeambukizwa VVU?

Jibu: Baada ya kutokea hayo, niliamua kutoroka nyumbani na kwenda kujihifadhi kwenye kituo cha kulea watoto yatima. Nilipokelewa na kuanza

Alibakwa na kuambukizwa Ukimwi

maisha mapya ambapo pia niliamua kuacha shule.

Niliendelea kukulia hapo. Lakini huko nako nilibakwa na mwanaume nisiyemjua. Alinivamia nje kidogo ya kituo chetu. Baada ya miaka saba tangu nibakwe nikaona afya yangu inaanza kutetereka polepole, nilikuwa naumwa homa mara kwa mara, kupungua uzito na kukohoa. Niliamua kwenda hospitali kupimwa na ikagundulika kuwa nimembukizwa tayari.

Swali: Matokeo ya vipimo uliyatarajia na je, ulifahamu kuwepo kwa ugonjwa huo?

Jibu: Kamwe sikuyatarajia, niliona kwa umri wangu mdogo, magonjwa kama Ukimwi hayanihusu. Nililia sana. Nilikata tamaa na kuona dunia yangu imefika mwisho.

Nilijawa na mawazo mengi, nikataka kujjua ili niondoke mapema duniani na nisije kuteseka kwa Ukimwi baada ya kuamini jamii itanikataa kwa unyanyapaa. Mawazo haya yaliendelea kwa muda wa miezi mitano, na kila siku

uzito wangu ulipungua kwa sababu ya msongo wa mawazo.

Lakini siku moja, miaka 10 iliyopita, niliamua kwenda hospitali tena na kuanza dawa za kufubaza virusi vya ukimwi, kwani natambua kwamba hakuna tiba kabisa.

Hospitalini walinfanyia uchunguzi na kubaini kwamba nahitaji kuanza kumeza ARVs, dawa za kupunguza makali ya ugonjwa huo. Tangu kipindi hicho hadi sasa, sijarudi nyuma na afya yangu inaimarika kila uchao, si unaona nakuwa mrembo zaidi! (anacheka).

Swali: Umesema una watoto watatu, wako salama, maana uliwapata wakati tayari umegundua kwamba umeambukizwa?

Jibu: Hawa watoto wote wako salama kabisa. Hawana maambukizi na vyeti vyao vya VVU hivi hapa kutoka hospitali mbili tofauti - (anaonyesha vyeti hivyo).

Swali: Umesema una mume, je, ana maambukizi kama wewe?

Jibu: Kama walivyo watoto wangu,



Alibakwa na kuambukizwa Ukimwi

na baba yao pia hana maambukizi. Hajaambukizwa na sitarajii apate mambukizi kutoka kwangu, kwa kuwa wote nawalinda.

Swali: Nawalindaje?

Jibu: Nawalinda kwa kutumia ARVs kila siku. Unajua unapotumia vidonge vya kufubaza VVU, mara nyingi, virusi vinakosa nguvu, vinashindwa kuongezeka, hivyo kunakosekana mwana wa kuambukiza wengine. Hatimaye unakuwa na msongamano mdogo wa VVU kwenye damu (low viral load count), kiasi kwamba huwezi kumwambukiza mtu.

Mume wangu na watoto wangu wamekuwa msaada mkubwa kwangu. Huwa wananikumbusha kumeza dawa kila unapofika muda. Watoto wangu, hasa huyu mkubwa—mwenye miaka 8—ananiletea dawa. Baba yao naye kila akitoka kazini lazima anikumbushe. Sasa dawa zimekuwa sehemu ya maisha yangu. Nimezoea kabisa.

Swali: Wakati unaanza uhusiano na mume wako alijua hali yako ya VVU?

Jibu: Hapana, hakujuu, nami sikutaka kuwa na papara kumwambia kwani nilikuwa natafuta muda muafaka wa kufanya hivyo.

Siku moja alikuja kunichukua nilipokuwa naishi - kwani baada ya kutoka kwenye kituo cha watoto yatima, nilipanga chumba. Tulitoka na kwenda matembezini, na huko ndiyo nilimweleza kuhusu hali yangu ya kuwa na VVU.

Alikosa nguvu baada ya kusikia kwamba nina maambukizi, aliinama kwa muda, lakini baadaye aliinua kichwa chake na kuonekana machozi yakimlengalenga. Nilimfahamisha kuwa nilikuwa na uhakika kuwa nitamlinda hata kama tukifanya ngono siwezi kumdhuru. Hatimaye akatamka... “usijali, nitaendelea kuwa nawe.” Baada ya hapo nilianza kumweleza kilichotokea.

Lakini hatukuwa tumefanya ngono kabla ya hapo, kwani nilitaka awe na uamuzi ulio huru kabisa kabla ya kuanza

uhusiano wa kimapenzi na mtu mwenye VVU.

Aliikubali hali yangu na tuliendelea hadi leo ambapo tuna watoto watatu na familia bora yenye furaha tele. Yeye na watoto wako salama.

Swali: Afrika ina watu milioni 37 wenye mambukizi na milioni 8 wako Afrika Kusini, nchini mwako, unawafikiaje hawa?

Jibu: Kama nilivyokueleza, vita dhidi ya Ukimwi naipigana kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Lakini pia natumika zaidi kutoa elimu kupitia matamasha mbalimbali, huko nakutana na vijana, kila nikisimama, wao wanaelimika na kujeepusha na maambukizi na wale walioambukizwa tayari, nawatia moyo na kuwasisitiza kuwa kupata Ukimwi siyo mwisho wa dunia. Kwamba maisha yapo tu hata baada ya kuambukizwa, kikubwa ni kujitunza na kufuata masharti ya wataalamu wa afya.

Swali: Vipi kuhusu tatizo la unyanyanjaa?

Jibu: Hapo awali baada ya watu kugundua kwamba nina maambukizi ya VVU walianza kunitenga. Unajua niliamua kuweka wazi mwenyewe kwenye mitandao ya kijamii. Lakini, baadaye nimezoeleka na nina marafiki dunia nzima. Kuna wachache wananinyanyapaa, lakini wengi wananiona shujaa. Hata wewe ni rafiki yangu kutoka Tanzania. Karibu!

Swali: Nini falsafa yako katika mapambano haya?

Jibu: Virusi viko ndani yangu, havinipi chakula, haviipii kodi, sviogopi. Mimi ndiye naviongoza. Havinitishi kamwe.

Naomba waathirika wengine wote waibebe hii falsafa. Na kama bado mtu hajaambukizwa, basi ajilinde ama kwa kujizuia, au kwa kufanya ngono salama kwa kutumia kondomu kila wakati, au kujenga mahusiano na mpenzi mmoja asiye na maambukizi.

Makala haya ya ana kwa ana yalichapishwa kwa mara ya kwanza na Mwanahalisionline.

Tendo la ndoa na umoja wa kimwili

Na Deusedith KAHANGWA

TAYARI tumeona kwamba, “mwili mmoja wa kibayolojia,” kama vile mwili wa mbuzi, unazo sifa kadhaa zinazotuwezesha kuhesabu mwili huo kama kitu kimoja kisichogawanyika wakati wa mchakato wa kuhesabu viumbehai. Sifa hizo ni kama ifuatavyo:

Mosi, anwani moja ya makazi ya viungo vya mwili ambayo ni endelevu (continuous spatial unity); pili, anwani moja ya majira ya viungo vya mwili ambayo ni endelevu (continuous synchronic unity); tatu, umri mmoja wa viungo vya mwili (diachronic unity);

Nne, uwezo wa mwili kujaza nafasi yote unayoishikilia, na hivyo kufukuza vitu baki kutoka katika makazi yake ya kijiografia; tano, uwepo wa mahusiano ya kietiolojia kati ya sehemu za mwili, katika namna ambayo inafanikisha lengo moja la kibayolojia; sita, uwepo wa mfumo wa neva mmoja unaoratibu utendaji wa viungo baki vya mwili;

Saba, mwili unaokubali viraka vya ngozi kutoka kwenye ngozi yake pekee na kukataa viraka vya ngozi kutoka kwenye ngozi ya kiumbe kingine; nane, kuwepo kwa vinasaba vyenye muundo na maudhui ya aina moja; tisa, mwili huo kuzaliwa kwa njia ya ngono na hatimaye kuzaa watoto wanaofanana na mzazi kwa njia ileile; na kumi, mwili huo kuwa na sifa ya kuitwa memba wa tabaka la viumbe fulani vya kibayolojia, badala ya kuwa tabaka la viumbe fulani vya kibayolojia.

Kama hivi ndivyo, sasa swali linazuka: Je, jozi ya mke na mume, inaunda “mwili mmoja wa kibayolojia” (one biological body) kama ambavyo mwili wa mbuzi unaunda mwili mmoja wa kibayolojia?

Njia nyingine ya kufanya udadisi huu wa kifalsafa ni kuuliza hivi: Je, uoganizimalia wa kibayolojia (biological organizationality) ni sifa mojawapo katika maisha ya mke na mume kama wakichukuliwa kama jozi moja ya



Aristotle

watendaji?

Tathmini yangu kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa uoganizimalia katika maisha ya jozi ya mke na mume ni kama ifuatavyo:

Mosi, viungo vya mwili wa jozi ya mke na mume havina anwani moja ya makazi na majira ambayo ni endelevu (spatial discontinuity). Wakati mke anapokuwa ofisini, mume anakuwa nyumbani; wakati mke yuko jikoni, mume yuko sebuleni; wakati mke yuko shuleni, mume yuko kanisani; na kwa ujumla, wakati mwingi, kila nusu ya jozi ya mke na mume inakuwa na makazi yake katika wakati ule ule, kiasi kwamba hawawezi kuhesabiwa kitu kimoja, kama zoezi ka kuhesabu likifanyika.

Mbili, viungo vya jozi ya mke na mume vina umri unaokatika katika (temporal discontinuity).

Mke na mume kama, kama jozi ya watu wanaojamiiana, ni ushiririka unaozaliwa na kufa ndani ya umri wa wastani wa dakika tano.

Baada ya hapo, ushirika huo utazaliwa tena kwenye raundi nyingine ya dakika kama hizo, ama siku hiyo, wiki hiyo, mwezi huo, au zaidi ya hapo.

Nje ya tendo la ngono jozi ya mke na mume ni miili miwili inayoshirikiana katika kazi za kawaida kama ilivyo katika jumua zingine.

Aidha, wakati viungo vya mwili wa mke vina umri mmoja kwa sababu ya

Tendo la ndoa na umoja wa kimwili

Inatoka Uk. 20

tarehe ya kuzaliwa ya mwanamke; viungo vya mwili wa mume vina umri mwingine kwa sababu ya tarehe ya kuzaliwa ya mwanamume.

Tatu, jozi ya mke na mume inao uwezo wa mwili wake kujaza nafasi yote unayoishikilia, na hivyo kufukuza vitu baki kutoka katika makazi yake ya kijiografia (spatial continuity).

Ukiondoa habari ya safari za hapa na pale, alipo mke hawezi kukaa mwanamke mwingine, alipo mume hawezi kukaa mwanamume mwingine.

Nne, wakati wa tendo la kujamiiana, ambalo huchukua wastani wa dakika tano, jozi ya mke na mume inaonyesha uwepo wa mahusiano ya kietiolojia kati ya sehemu za mwili, katika namna ambayo inafanikisha lengo moja la kibayolojia (teleological unity).

Kujamiiana ni hatua ya kwanza ya mchakato mrefu wa uzazi, wenye kuhusisha urutubisho, utungaji wa mimba, kulea mimba, kuzaa, kunyonyesha, na kulea mtoto.

Tano, jozi ya mke na mume haina mfumo wa neva mmoja unaoratibu utendaji wa viungo baki vya mwili.

Badala yake kuna mifumo miwili ya neva, mke akiwa na wake na mume vivo hivo.

Sita, jozi ya mke na mume haina mwili unaokubali viraka vya ngozi kutoka kwenye ngozi yoyote kati yao. Yaani, ukitumia ngozi ya mume kuweka kiraka kwenye ngozi ya mke hakishiki. Vivyo hivyo, ukitumia ngozi ya mke kuweka kiraka kwenye ngozi ya mume hakishiki.

Saba, jozi ya mke na mume haina vinasaba vyenye muundo na maudhui ya aina moja. Mke ana vinasaba vya kipekee, na vivyo hivyo mume.

Nane, jozi ya mke na mume, kama jozi ya watu wanaojamiiana, yaani “copulating pair,” ambayo hapa tuuite “kopyulanti” (copulant) haina sifa ya kuzaliwa kwa mpigo kama kiumbe kimoja kwa njia ya ngono kama ambavyo



Ndoa

hutokea kwa mapacha.

Vivyo hivyo, “kopyulanti” hana uwezo wa kuzaa “kopyulanti” mwingine kwa njia ya ngono.

Na tisa, jozi ya mke na mume haina sifa ya kuitwa memba wa tabaka la vitu vyenye mwili mmoja wa kibayolojia, kwani yenyewe ni tabaka la vitu viwili, kila kimoja kikiwa na mwili mmoja wa kibayolojia.

Hivyo, basi, sasa natoa jawabu hasi kwa swali lifuatalo: Je, jozi ya mke na mume, ni “mwili mmoja wa kibayolojia” kama ambavyo mwili wa mbuzi ni mwili mmoja?

Yaani, jawabu langu ni kwamba jozi ya mke na mume siyo “mwili mmoja wa kibayolojia,” kwa kuwa haikidhi matakwa ya vigezo vyenye umuhimu na ulazima kwa ajili ya kuthibitisha uwepo wa umwa wa mwili wa kibayolojia.

Mpaka hapo, mtu sasa anaweza kuuliza: kama hivi ndivyo, ni katika muktadha gani tunaambiwa kuwa mke na mume “siyo wawili tena bali wamekuwa mwili mmoja”?

Jawabu langu ni kwamba, haya ni maneno ya ufananisho tu (metaphorical meaning), na sio yenye kubeba maana sisisi (literal meaning).

Kwa sababu hizi, hakuna mwili mmoja unaovunjwa na kingamimba, kama ambavyo baadhi ya wanateolojia wanafikiri na kufundisha kwa miaka 2000

Tendo la ndoa na umoja wa kimwili*Inatoka Uk. 21*

sasa.

Na hivyo, Sera ya Afya ya Taifa ya 2017 ikabadilishwa ili kuongeza kipengele cha kingamimba kama mbinu ya kupanga uzazi inayoiwezesha jozi ya bibi na bwana kuipiga chenga mimba na kufanikisha utulivu wa kimwili na kiakili.

Mapingamizi na majibu yake

Baada ya kusema hayo sasa napenda kujibu baadhi ya mapingamizi ninayoyakisia dhidi ya hoja yangu kama ilivyowasilishwa hapo juu.

Mosi, mtu anaweza kusema kwamba, pamoja na uzuri wa hoja hii, lakini bado, mke na mume wanageuka “mwili mmoja wa kibayolojia” pale wanapokuwa wamefanikiwa kupata mtoto.

Nasema hapani. Badala yake, jozi ya mke na mume ni jozi ya watendaji wanaoshirikiana kutekeleza tendo la ngono ambalo, mara nyingi, huwa ni hatua ya kwanza katika mchakato mrefu wa urutubishaji, mimba, na uzazi.

Mtoto anapozaliwa umoja wa kimwili kati ya baba na mama hutokea kwa njia ya mzunguko kupitia kwa mtoto. Lakini, bado baba na mama wanabaki ni miili miwili ya kibayolojia.

Pili, mtu anaweza kusema kuwa vigezo vya kutambulisha “umoja wa mwili wa kibayolojia” vina dosari kwa kuwa umetaja “muundo mmoja wa kinasaba” wakati mapacha sisi wanayo sifa hiyo wakati wanayo miili miwili tofauti.

Najibu kwamba, seti ya vigezo 10 nilivyovitaja kama utambulisho muhimu na wa lazima kwa ajili ya kubainisha umoja wa mwili wa kibayolojia vinavyofanya kazi pamoja.

Yafaa kueleza hapa kuwa, upekee wa kibayolojia (biological individuality) kuhusiana na kiumbehai kama vile mbuzi, huwa na sifa za aina mbili.

Kuna sifa za ndani ya mwili wa kiumbe (intrinsic properties) na sifa za nje ya mwili wa kiumbe (extrinsic properties).

Mfano, idadi na muundo wa vinasaba vya pacha aitwaye Doto ni sifa ya ndani ya mwili wakati makazi ya pacha aitwaye

*Ndoa*

Kulwa ni sifa iliyo nje ya mwili wa Doto.

Sifa za ndani na nje zikiunganishwa zinatuwezesha kuwatofautisha mapacha sisi. Seti yangu yenye sifa kadhaa inajumuisha sifa za ndani na nje ya miili ya viumbehai.

Tatu, mtu anaweza kusema kuwa, hoja yangu ni mbinu ya kufungua milango ya anasa ya ngono holela. Nakataa. Nijuavyo, mbali na ukweli kwamba, tendo la ngono ni hatua ya kwanza ya mchakato wa uzazi, na hivyo tendo la uzazi (procreative act), lakini pia, tendo la ngono ya jenitalia kwa jenitalia ni hatua ya kwanza katika mchakato mwingine wa kutengeneza upya umoja wa mwili na akili (psychosomatic integration).

Mchakato huu wa matengenezo mapya, unaanzia katika mduara wa mwitiko chanya wa kimapenzi (sexual response cycle) wenye hatua zifuatazo: msisimko wa jenitalia, msuguano wa jenitalia, mshindo, kushusha pumzi, na uzalishaji wa homoni za faraja kama vile homoni za “oxytocin, serotonin, dopamine, endorphines.”

Kazi ya homoni hizi ni kuuzalisha upya umoja wa mwili na roho, na hivyo kukarabati amani ya moyo.

Kila hatua katika mduara huu inaambatana na anasa ya jenitalia kama ambavyo kula chakula huambatana na anasa ya ulimi.

Lakini, mwisho wa siku, kama ambavyo anasa ya ulimi husindikiza tunu chanya ya lishe (the good of nutrition), vivyo hivyo, anasa ya jenitalia husindikiza tunu chanya ya utulivu wa kiakili na kimwili (the good of psychosomatic integrity).

Mwamuzi aweka rekodi



MWAMUZI Ramadhan Kayoko jana aliweka rekodi kwa mechi za ‘dabi’ za hivi karibuni baada ya ‘kugawa’ jumla ya kadi za njano tisa, wakati Simba na Yanga zilipopambana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo, Kayoko aligawa kadi tano za njano kwa Simba na nyingine nne kwa Yanga katika pambano hilo la 109 katika Ligi ya Bara tangu mwaka 1965.

Wachezaji wa Simba waliopewa kadi hizo ni Israil Mwenda, Mohammed Hussein ‘Tshabalala’, Mzamiru Yasin, Habib Kyombo na Augustine Okrah, wakati kwa Yanga waliolimwa ni Djuma Shaban, Stephane Aziz KI, Khalid Aucho na Feisal Salum ‘Fei Toto’.

Ilikuwa ni miujiza tu kwa mwamuzi huyo kutoa kasi nyekundu kwa namna wachezaji wa timu zote walivyoonkana kukamiana na kuchezea ubabe katika dakika zote 90. Jonas Mkude angeweza kutolewa kwa kadi ya pili ya njano mapema kabla ya Fei Toto aliyekuwa na njano kwa kucheza faulo ambayo ilitahili kadi ya pili ya njano.

Mechi iliyokuwa inashikilia rekodi kwa kadi nyingi za dabi lilikuwa ni lile la Mei 6, 2012 wakati Yanga ikipigwa mabao 5-0 ambapo mwamuzi Hashim Abdallah alitoa njano saba na penalti tatu na kuifanya Simba ikabidhiwe taji lao la ubingwa kwa shangwe.

MwanaSpoti

PICHA KUBWA



Pundamilia wakivinjari ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti hivi karibuni kama walivyokutwa na mpigapicha wa hifadhi hiyo. Eneo la hifadhi hiyo ni miongoni mwa vivutio vingi vya utalii nchini Tanzania.

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

